



National Council of NGOs

6 Kiko Avenue (3rd floor) Mikocheni A
P.O.BOX 34163, Tell +255222772402
Dar es Salaam, Tanzania
Email: info@nacongo.or.tz
www.nacongo.or.tz

TAARIFA KWA UMMA

Dodoma, 28/4/2021

Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Ndugu Wadau wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali na wadau wa Maendeleo, Ndugu Waandishi wa Habari itifaki imezingatiwa.

Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (The National Council of Non-Governmental Organizations – NaCoNGO) ni chombo kilichoundwa kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) Namba 24 ya mwaka 2002, pamoja na marekebisho yake kupitia Sheria Namba 11 ya mwaka 2005 na Sheria Namba 3 ya mwaka 2019. Kifungu cha 25 (2) cha Sheria hiyo ya NGOs imeipa NaCoNGO mamlaka ya kuratibu shughuli na kusimamia Kanuni za Maadili kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini. Katika kutekeleza shughuli zake, Baraza linaongozwa na Kanuni za usimamizi wa Baraza [NonGovernmental Organizations (The National Council Operational) Regulations] ambazo zinatambua na kuainisha Viongozi na Vyombo vinavyounda Baraza na majukumu yake, vikiwemo Mkutano Mkuu wa Baraza na Kamati Tendaji.

Kwanza Kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna alivyotuwezesha kwa Idadi hii ya kuridhisha kufika katika Mkutano huu Muhimu,

Baraza kwa niaba ya Sekta ya NGOs nchini, linazidi kuungana na Watanzania wote kumshukuru Mungu kutupa hali ya uvumilivu katika kipindi chote cha Msiba Mkubwa uliolikumba Taifa tr 17.03.2021 ambapo tulimpoteza Mzalendo wetu wa mfano namba moja Mhe: Hayati Dr John Pombe Joseph Magufuli, tumekuwa na utulivu kama Taifa, Familia ya Hayati, na Mrithi wake Mhe; Raisi Samia Suluhu Hassan, Baraza linaendelea kutoa Pole kwa Familia Ya Hayati hususani Mama Janeth Magufuli, Watoto wa Marehemu, Mhe: Raisi Samia Suluhu Hassan na Watanzania wote kwa ujumla wake. Mwenyezi Mungu aendelee kuiweka Roho ya Marehemu Mahala pema peponi.

KUHUSU MCHAKATO WA MABORESHO YA KANUNI ZA BARAZA

Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo Ya Kiserikali, kwa kushirikiana na wadau wake ikiwemo Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo Ya Kiserikali, iliona udhaifu wa Kanuni zilizokua zinaliongoza Baraza na kuazimia kuzifanyia Maboresho, zikiwemo Kanuni za Uchaguzi.

Mchakato wa Maboresho hayo uliruhusiwa na kuelekezwa na Bodi tr 03.12.2019 na kuanza kushughulikiwa na Baraza.

Hatua ya kwanza ilikua ni kusitisha upokeaji wa Ada za Wadau wake ambazo pia kwenye kanuni za awali zilihiti marekebicho, Mchakato huo ulianza kwa kukusanya maoni kwa Wadau, Mchakato ambao ulikamilika mwezi wa Januari 2021 kwa kuthibitishwa na wadau, baadae hatua iliyofanyika ni kupitishwa na Baraza katika kikao kilichofanyika jana Hapa Morena Hotel Dodoma, ambapo Kanuni zimekamilika na hatua inayofuata ni kuzikabidhi Kanuni Mpya za Baraza kwenye Bodi ya Uratibu wa NGOs ambapo ikiwapendeza watazipitisha na kuzichapa kwenye Gazeti la Serikali.

Kwakua ucheleweshaji huu wote, pamoja na sababu zingine, ilikua ni ukosefu wa fedha kwa wakati za kutosha kujiendesha kuzipitia kanuni hizo kwa kushirikisha wadau. Katika kikao hicho hapa Dodoma, **Baraza limekuja na maazimio yafuatayo.**

- 1. KUWE NA KIKAO KAZI BAINA YA BARAZA NA BODI KITAKACHO JADILI NA KUTOKA NA MAAZIMIO YENYE MANUFAA KWA SEKTA YA NGOs NCHINI.**
- 2. UCHAGUZI WA BARAZA UFANYIKE KWA KUFUATA MPANGO KAZI WA BARAZA NA KANUNI MPYA KUANZIA NGAZI YA WILAYA, MKOA NA TAIFA, BAADA YA KANUNI MPYA ZA UCHAGUZI NA UENDESHAJI WA BARAZA KUTANGAZWA NA BODI YA URATIBU KATIKA GAZETI LA SERIKALI NA WADAU WA UCHAGUZI HUO KUWA NA TAARIFA.**
- 3. TUNAIOMBA SERIKALI IHARAKISHE MCHAKATO WA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YALIYOFIKIWA KATIKA MKUTANO KAZI WA BAINA YA SEKTA YA NGOs KWA UPANDE MMOJA NA WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO KWA UPANDE WA PILI.**

4. **CHOMBO CHENYE MAMLAKA YA KUTOA TAMKO KWA NIABA YA SEKTA YA NGOs NCHINI, NI BARAZA LA TAIFA LA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NaCoNGO), MATAMKO YA MITANDAO NA MASHIRIKA YALENGE MIPAKA YAO NA SIO KWA NIABA YA SEKTA YA NGOs NCHINI, TUNAOMBA SERIKALI ISİYACHUKULIE MATAMKO YALIYOTOLEWA NA MITANDAO YA MASHIRIKA KADHAA KUWA NI TAMKO KWA NIABA YA SEKTA YA NGOs .**

5. **NaCoNGO KWA KUSHIRIKIANA NA WIZARA MAMA IHUSISHWE KIKAMILIFU NA SERIKALI KATIKA HATUA ZA UUNDWAJI WA MIONGOZO AU SERA ZINAZOHUSU MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI.**

6. **SHERIA ILIYOUNDA BARAZA ILILENGA BARAZA KUJISIMAMIA NA KUJIENDESHA LENYEWE, BARAZA LILIAMUA KUTOKUPOKEA ADA KWA WADAU WAKE KWA MUDA WOTE WA MABORESHO YA KANUNI ZAKE, SASA KANUNI ZIMEKAMILIKA NA KUAZIMIA KUWA NA TOZO ZIFUATAZO ZITAKAZOANZA KUTEKELEZWA MWEZI MAY 2021 ILI KULIREJESHA BARAZA KATIKA UTENDAJI WAKE:-**

TOZO HIZO NI

- **INGO = USD 250**
- **GRANT MAKERS NGO TSHS 400,000/=**
- **NATIONAL NET WORKS/COALITION 100,000/=**
- **NGO LOCAL 30,000/=**

IMETOLEWA NA



**NICHOLAUS ZACHARIA
MWENYEKITI**

BARAZA LA TAIFA LA MASHIRIKA YASIYOKUA YAKISERIKALI (NaCoNGO)